

## Average Insha KCPE 2008

Anza kwa: Wingu kubwa jeusi lilitokea upande wa mashariki. Baadaye matone mazito mazito .....

### DALILI YA MVUA NI MAWINGU

Wingu kubwa jeusi lilitokea upande wa mashariki. Baadaye matone mazito yalianza kutunyesheya, yasiyojulikana yametokea - upande gani wa dunia. Basi muda si muda hayakuwa ni matone tena ila ilikuwa ni mvua ya masika ambayo iliwaathiri wengi na kusababisha mafuriko na hata vifo vya watu kadha wa kadha.

Wanalugha hawakutuchezea shera walipolonga dalili za mvua ni mawingu, kwani wingu kubwa jeusi lilipotokea upande wa mashariki na baadaye matone mazito yakaanza kutunyesheya. Kwa upande wetu sisi tulidhani kuwa ni dalili za upepo mwanana unaovuma kutoka mashariki. Kumbe lo! zilikuwa ni dalili za mvua.

Mvua hiyo iliyongesha kwa muda wa saa mbili hivi ilikuwa ya uharibifu, kama nilivyo kuwa nimetaja hapo awali. Haya hapa yaliyohudhuriwa kutokana na uharibifu huo, mafuriko yalikuwako, mifugo ikaathirika na kukufa, mimea ikaathirika pia kwa kufunika na maji, huku pia wanadamu

waliathirika pakubwa na hata wengine wao  
wakaenda jongomeo.

Mbali na hayo shule pia zililazimika kufunga  
hadi hali ingerejea kuwa ya kawaida, afisi  
nyingine za serikali na za uma zililazimika pia  
kufunga hadi hali hiyo ingekuwa shwari kabisa.

Kutokana na mafuriko hayo watu walilazimika  
kuhama na kutaputa hifadhi. Kwa hivyo basi  
wengine wao walihamia kwenye jamii zilizokuwa  
mbali kutokana na hapo ambazo walizokuwa  
nazo na ukoo. Huku kupata hifadhi ilikuwa  
ni shida mno, kumwona mtu akiwa amepata  
hifadhi alikuwa amefanya kazi ya ziada.

Basi mtu alilazimika kufanya juu chini ili  
aweze kuvokoa uhai wake. Watu walijaribu  
kwa udi na uvumba lakini wapi? Walilazimika  
kuhama kwenye kambi ya polisi na kunadi  
kuwa waledi wa lugha hawakutupiga mafumbo  
waliposema ukupaaye kwa dhiki ndiye rafiki.  
Huku walikuwa kwenye dhiki lakini hawakupata  
rafiki ambaye aliwafaa.

Walipokimbilia kwenye kambi ya polisi ndipo  
walipopata hifadhi iliyowafaa. Na juu ya haya  
yote ilikuwa tu ni mafuriko yaliyosababishwa  
na mvua, na huku ndipo wanalugha walinadi  
dalili ya mvua ni mawingu.

Alama iliyotuzwa 22.

Mwandishi wa insha hii anielewa mada na amejaribu kuishughulikia. Hata hivyo amefanya makosa mengi ya kisarufi na tahajia. Pia insha yake ni fupi na hoja zake ni chache mno, yaani hakuzikuza kuifanya hadithi iwe ndefu kiasi. Insha yake in kavu haijapambwa kwa semi.